# 1 Wathesalonike

### *Salamu*

1 Paulo, Silvano* na Timotheo.
Kwa kundi la waumini la Wathesalonike,
ninyi mlio ndani ya Mungu, Baba† yetu, na
ndani ya Bwana wetu Isa Al-Masihi.
Neema iwe kwenu na amani.

### *Shukrani kwa ajili ya imani ya Wathesalonike*

2 Siku zote tunamshukuru Mungu kwa ajili
yenu ninyi nyote, tukiwataja kwenye maombi
yetu daima.
3 Tunaikumbuka daima kazi yenu ya imani
mbele za Mungu aliye Baba yetu, taabu yenu
katika upendo na saburi yenu ya tumaini katika
Bwana wetu Isa Al-Masihi.
4 Ndugu zetu mnaopendwa na Mungu, kwa
kuwa tunajua kwamba Mungu amewachagua,
5 kwa sababu ujumbe wetu wa Injili haukuja
kwenu kwa maneno matupu bali pia ulid-
hihirishwa katika nguvu na katika Roho wa
Mungu, tena ukiwa na uthibitisho kamili, kama
vile ninyi wenyewe mnavyojua jinsi tulivyoe-
nenda kati yenu kwa ajili yenu.
6 Nanyi mkawa wafuasi wetu na wa Bwana
Isa, ingawa mlipata mateso mengi, mlilipokea lile
Neno kwa furaha katika Roho wa Mungu.

---

* **1:1** yaani *Sila* † **1:1** Kwa mwanadamu, Mwenyezi Mungu ni Baba kupitia uhusiano unaopatikana katika kumtumaini Isa Al-Masihi.

7 Hivyo ninyi mkawa kielelezo kwa waumini
wote katika Makedonia na Akaya.
8 Kwa maana kutoka kwenu neno la Bwana Isa
limesikika, si katika Makedonia na Akaya tu, bali
pia imani yenu katika Mungu imejulikana kila
mahali, kiasi kwamba hatuna haja ya kusema
chochote juu yake.
9 Kwa maana watu wa maeneo hayo wenyewe
wanaeleza jinsi mlivyotupokea na jinsi mlivy-
omgeukia Mungu mkaacha sanamu, ili kumtu-
mikia Mungu aliye hai na wa kweli,
10 na ili kumngojea Mwanawe kutoka mbin-
guni, ambaye Mungu alimfufua kutoka kwa
wafu: yaani Isa, yeye aliyetuokoa kutoka ghad-
habu inayokuja.

# 2

### *Huduma ya Paulo huko Thesalonike*

1 Ndugu zangu, kwa kuwa ninyi wenyewe
mnajua kwamba kuja kwetu kwenu hakukuwa
bure,
2 kama vile mjuavyo, tulikuwa tumeteswa na
kutukanwa huko Filipi, lakini hata hivyo, kwa
msaada wa Mungu wetu, tulikuwa na ujasiri wa
kuwaambia Injili ya Mungu ingawa kulikuwa na
upinzani mkubwa.
3 Kwa maana himizo letu halikutokana na hila
wala nia mbaya au udanganyifu.
4 Kinyume chake, tulinena kama watu
tuliokubaliwa na Mungu tukakabidhiwa Injili.
Sisi hatujaribu kuwapendeza wanadamu bali
kumpendeza Mungu, yeye ayachunguzaye
mawazo ya ndani sana ya mioyo yetu.

5 Kama mnavyojua, hatukuja kwenu kwa ma-
neno ya kujipendekeza au maneno yasiyo ya
kweli ili kuficha tamaa mbaya; Mungu ndiye
shahidi yetu.
6 Hatukuwa tukitafuta sifa kutoka kwa
wanadamu, wala kutoka kwenu au kwa mtu
mwingine yeyote, ingawa kama mitume wa
Al-Masihi tungeweza kuwa mzigo kwenu.
7 Lakini tulikuwa wapole kati yenu, kama vile
mama anawatunza watoto wake wadogo.
8 Tuliwapenda sana, kiasi kwamba tulifurahia
kushirikiana nanyi, si Injili ya Mungu tu, bali
hata maisha yetu, kwa sababu mlikuwa wa
thamani mno kwetu.
9 Ndugu zetu, mnakumbuka juhudi yetu na
taabu yetu. Tulifanya kazi usiku na mchana,
ili tusiwe mzigo kwa mtu yeyote tulipokuwa
tukiwahubiria Injili ya Mungu.

10 Ninyi wenyewe ni mashahidi na Mungu
pia, jinsi tulivyokuwa watakatifu, wenye haki
na wasio na lawama miongoni mwenu ninyi
mlioamini.
11 Maana mnajua kwamba tuliwatendea kila
mmoja wenu kama vile baba anavyowatendea
watoto wake.
12 Tuliwatia moyo, tukiwafariji na kuwahimiza
kuishi maisha yanayompendeza Mungu,
anayewaita katika ufalme wake na utukufu
wake.
13 Nasi pia tunamshukuru Mungu bila kukoma
kwa sababu mlipolipokea neno la Mungu
mlilosikia kutoka kwetu, hamkulipokea kama
neno la wanadamu, bali mlilipokea kama lilivyo

hasa, neno la Mungu, linalotenda kazi ndani yenu ninyi mnaoamini.
14 Kwa maana ninyi ndugu zetu, mlifanyika
wafuasi wa makundi ya waumini wa Mungu walio ndani ya Al-Masihi Isa katika Yudea. Mlipata mateso yale yale kutoka kwa watu wenu wenyewe kama vile waumini hao walivyoteswa na Wayahudi,
15 wale waliomuua Bwana Isa na manabii,
nasi wakatufukuza pia. Watu hao walimchukiza Mungu na tena ni adui wa watu wote,
16 wakijitahidi kutuzuia tusizungumze na watu
wa Mataifa ili wapate kuokolewa. Kwa njia hii wanazidi kujilundikia dhambi zao hadi kikomo. Lakini hatimaye ghadhabu ya Mungu imewafikia.

### *Paulo atamani kuwaona Wathesalonike*

17 Lakini ndugu zetu, tulipotenganishwa nanyi
kwa muda mfupi (ingawa kutengana huko kulikuwa kwa mwili tu, si kwa moyo), tulizidi kuwa na shauku kubwa kuwaona uso kwa uso.
18 Maana tulitaka kuja kwenu, hasa mimi
Paulo, nilitaka kuja tena na tena, lakini Shetani akatuzuia.
19 Kwa maana tumaini letu ni nini, au furaha
yetu, au taji letu la kujisifia mbele za Bwana wetu Isa Al-Masihi wakati wa kuja kwake? Je, si ni ninyi?
20 Naam, ninyi ndio fahari yetu na furaha yetu.

# 3

### *Timotheo atumwa Thesalonike*

1 Kwa hivyo tulipokuwa hatuwezi kuvumilia
zaidi, tuliamua tubaki Athene peke yetu.
2 Tukamtuma Timotheo ambaye ni ndugu
yetu na mtumishi mwenzetu wa Mungu katika
kuieneza Injili ya Al-Masihi, aje kuwaimarisha na
kuwatia moyo katika imani yenu,
3 ili mtu yeyote asifadhaishwe na mateso
haya. Mnajua vyema kwamba tumewekewa
hayo mateso.
4 Kwa kweli, tulipokuwa pamoja nanyi tuli-
waambia mara kwa mara kwamba tutateswa na
imekuwa hivyo kama mnavyojua.
5 Kwa sababu hii niliposhindwa kuvumilia
zaidi, nilimtuma mtu ili nipate habari za imani
yenu. Niliogopa kwamba kwa njia fulani yule
mjaribu asiwe amewajaribu, nasi tukawa tume-
jitaabisha bure.

### *Taarifa ya Timotheo ya kutia moyo*

6 Lakini Timotheo amerejea kwetu hivi sasa
kutoka kwenu, na ameleta habari njema kuhusu
imani yenu na upendo wenu. Ametuambia
kwamba siku zote mnatukumbuka kwa wema,
na kwamba mna shauku ya kutuona kama vile
sisi tulivyo na shauku ya kuwaona ninyi.
7 Kwa hiyo, ndugu zetu, katika dhiki na mateso
yetu yote tumefarijika kwa sababu ya imani
yenu.
8 Sasa kwa kuwa hakika tunaishi, kwa kuwa
ninyi mmesimama imara katika Bwana Isa.
9 Je, tutawezaje kumshukuru Mungu kiasi cha
kutosha kwa ajili yenu, kutokana na furaha
tuliyo nayo mbele za Mungu wetu kwa sababu
yenu?

10 Usiku na mchana tunaomba kwa bidii ili tu-
pate kuwaona tena na kujaza kile kilichopungua
katika imani yenu.
11 Basi Mungu wetu na Baba yetu mwenyewe
na Bwana wetu Isa atengeneze njia ya sisi kuja
kwenu.
12 Bwana Isa na auongeze upendo wenu na
kuuzidisha kati yenu na kwa wengine wote,
kama vile tulivyo na upendo mwingi kwenu.
13 Tunamwomba Mungu aimarishe mioyo yenu
ili msiwe na lawama katika utakatifu mbele za
Mungu wetu aliye Baba yetu wakati wa kuja
kwake Bwana wetu Isa pamoja na watakatifu
wote.

# 4

## *Maisha yanayompendeza Mwenyezi Mungu*

1 Na kuhusu mambo mengine, ndugu, tuliwa-
fundisha jinsi ya kuishi ili kumpendeza Mungu,
kama vile mnavyoishi. Sasa tunawaomba na
kuwasihi katika Bwana Isa mfanye hivi zaidi na
zaidi.
2 Kwa kuwa mnajua maagizo tuliyowapa kwa
mamlaka ya Bwana Isa.
3 Mapenzi ya Mungu ni ninyi mtakaswe, ili
mjiepushe na uasherati,
4 na kila mmoja wenu ajifunze kuutawala
mwili wake mwenyewe katika utakatifu na hes-
hima,
5 bali si kwa tamaa mbaya kama watu wa
Mataifa wasiomjua Mungu.
6 Katika jambo hili mtu asimkosee ndugu
yake wala kumlaghai. Kwa kuwa Mwenyezi

Mungu ni mlipiza kisasi katika mambo haya yote,
kama vile tulivyokwisha kuwaambia mapema na
kuwaonya vikali.
7 Kwa maana Mungu hakutuitia uchafu, bali
utakatifu.
8 Kwa hiyo, mtu yeyote anayekataa
mafundisho haya hamkatai mwanadamu, bali
anamkataa Mungu anayewapa ninyi Roho wake
Mtakatifu.
9 Sasa kuhusu upendo wa ndugu hamna haja
mtu yeyote kuwaandikia, kwa maana ninyi
wenyewe mmefundishwa na Mungu kupendana.
10 Nanyi kwa kweli mnawapenda ndugu wote
katika Makedonia nzima. Lakini ndugu, tu-
nawasihi mzidi sana kuwapenda.
11 Jitahidini kuishi maisha ya utulivu, kila mtu
akijishughulisha na mambo yake mwenyewe na
kufanya kazi kwa mikono yake, kama vile tulivy-
owaagiza,
12 ili maisha yenu ya kila siku yajipatie heshima
kutoka kwa watu walio nje, ili msimtegemee mtu
yeyote.

### *Kurudi kwake Bwana Isa*

13 Lakini ndugu, hatutaki mkose kujua kuhusu
wale waliolala katika mauti, ili msihuzunike
kama watu wengine wasiokuwa na tumaini.
14 Tunaamini kwamba Isa alikufa na kufu-
fuka. Na kwa hivyo, tunaamini kwamba Mungu
atawaleta pamoja naye wale waliolala katika Isa.
15 Kulingana na neno la Bwana Isa mwenyewe,
tunawaambia kwamba sisi ambao bado tuko hai,
tuliobaki hadi kuja kwake Bwana Isa, hakika
hatutawatangulia waliolala katika mauti.

16 Kwa maana Bwana Isa mwenyewe atashuka kutoka mbinguni, akitoa amri kwa sauti kuu, pamoja na sauti ya malaika mkuu, na sauti ya tarumbeta ya Mungu. Nao waliokufa wakiwa katika Al-Masihi watafufuka kwanza.
17 Baada ya hilo sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu ili kumlaki Bwana Isa hewani, hivyo tutakuwa pamoja na Bwana Isa milele.
18 Kwa hiyo farijianeni kwa maneno haya.

# 5

### *Kuweni tayari kwa siku ya Bwana*

1 Basi ndugu, hatuna haja ya kuwaandikia kuhusu nyakati na majira,
2 kwa kuwa mnajua vyema kwamba siku ya Mwenyezi Mungu itakuja kama mwizi anavyokuja usiku.
3 Watu wanaposema, "Kuna amani na salama," maangamizi huwajia ghafula, kama vile uchungu unavyomjia mwanamke mwenye mimba; nao hakika hawatatoroka.
4 Bali ninyi, ndugu, hampo gizani hata siku ile iwakute ghafula kama mwizi.
5 Ninyi nyote ni wana wa nuru na wana wa mchana. Sisi si wana wa giza wala wa usiku.
6 Kwa hiyo basi, tusilale kama watu wengine wanavyolala, bali tukeshe na kuwa na kiasi.
7 Kwa kuwa wote wanaolala, hulala usiku, na wale wanaolewa, hulewa usiku.
8 Lakini kwa kuwa sisi ni wana wa mchana, basi tuwe na kiasi, tukijivika imani na upendo

kama dirii kifuani na tumaini letu la wokovu kama chapeo.
9 Kwa maana Mungu hakutuita ili tupate ghadhabu bali tupate wokovu kupitia kwa Bwana wetu Isa Al-Masihi.
10 Yeye alikufa kwa ajili yetu ili hata kama tuko macho au tumelala, tupate kuishi pamoja naye.
11 Kwa hiyo farijianeni na kujengana, kama vile mnavyofanya sasa.

### *Maagizo ya mwisho, na hitimisho*

12 Sasa tunawaomba, ndugu, waheshimuni wale wanaofanya kazi kwa bidii miongoni mwenu, wale ambao wana mamlaka juu yenu katika Bwana Isa na ambao wanawaonya.
13 Waheshimuni sana katika upendo kwa ajili ya kazi zao. Ishini kwa amani ninyi kwa ninyi.
14 Nasi twawasihi, ndugu, waonyeni walio wavivu, watieni moyo waoga, wasaidieni wanyonge na kuwavumilia watu wote.
15 Angalieni kuwa mtu asimlipe mwenzake maovu kwa maovu, bali siku zote tafuteni kutendeana mema ninyi kwa ninyi na kwa watu wote.
16 Furahini siku zote;
17 ombeni bila kukoma;
18 shukuruni kwa kila jambo, kwa maana haya ndio mapenzi ya Mungu kwa ajili yenu katika Al-Masihi Isa.
19 Msiuzime moto wa Roho wa Mungu.
20 Msiyadharau maneno ya unabii.
21 Jaribuni kila kitu. Yashikeni yaliyo mema.
22 Jiepusheni na uovu wa kila namna.
23 Mungu mwenyewe, Mungu wa amani, awatakase ninyi kabisa. Nanyi mhifadhiwe roho

zenu, nafsi zenu na miili yenu, bila kuwa na
lawama katika Bwana wetu Isa Al-Masihi.
24 Yeye aliyewaita ni mwaminifu naye atafanya
hayo.

25 Ndugu, tuombeeni.

26 Wasalimuni ndugu wote kwa busu takatifu.

27 Ninawaagiza mbele za Bwana Isa mhakik-
ishe kuwa ndugu wote wanasomewa barua hii.

28 Neema ya Bwana wetu Isa Al-Masihi iwe
nanyi. Amen.

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu

## The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

**Creative Commons License**

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: “Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible.” Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

“Biblica” ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

“Biblica” is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: "The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible."

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 20 May 2025 from source files dated 21 May 2025

72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d